# Haki ya Uwiano

## Sura ya 9

### Somo la Kusikiza: Agano Jipya 9

Shababa: Kuelewa jinzi anavyotaka Yesu, sisi kutumia mafunzo yake katika uhusiano wetu.

*Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.*

- Mathayo 5:19

Yesu anaendeleza matumizi ya mahubiri yake kwa kutoa taarifa mbili muhimu. Ya kwanza ni kuwa amekuja kutimiza sheria ya Mungu, na si kuiharibu. Ya pili ni kuwa haki ya wale wanaomfuata Yeye, inapaswa kuwa kuu hata kuliko ile ya waandishi na Mafarisayo, waalimu wa dini wa wakati huo, ambao haswa hawakuelewa Torati na kwanini Mungu aliipeana. Viongozi wa kidini walikuwa wamesahau kuwa Torati ilitengenezwa kwa ajili ya watu, na si watu kwa ajili ya Torati. Haki yao ilikuwa yote katika tabia za nje, na si kwa mioyo yao. Wafuasi wa Yesu wangekuwa na haki kuu zaidi na ya undani kwa sababu ilitoka moyoni.

Kisha Yesu anasema kuwa, ili kuwa sehemu ya suluhisho lake, sehemu ya jibu lake kwa maswali yao, wanafunzi wa Yesu wanapaswa kujua Neno la Mungu. Baada ya kutoa taarifa hizi kulingana na umuhimu wa maandiko katika maisha ya mwanafunzi, Yesu anawaonyesha namna ya kutumia mafundisho yake katika uhusiano wao. Uhusiano wa kwanza anaowafundisha ni uhusiano na ndugu au mwanafunzi mwenzake. Kisha anawafundisha mwitikio wa Mkristo kwa adui. Kisha anawaelezea jinzi ilivyo muhimu kwa wafuasi wake kushughulikia kipawa kizuri cha ngono katika njia ambazo Mungu anawaagiza. Ujumbe wa yesu unatusaidia kuelewa kuwa shina la dhambi huanza mapema kabla dhambi yenyewe kutendwa. Yesu anatufundisha kuwa tunaweza miliki tamaa zetu kabla hazijatusukuma kumuasi Mungu.

1. Ukweli au uongo? Si muhimu kwa Wakristo kuwa wenye haki.

2. Ukweli au uongo? Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa Agano la Kale halikuwa tena la muhimu kwa Ufalme wake.

3. Ukweli au uongo? Mafundisho ya Yesu hayakupinga Torati ya Musa.

4. Ukweli au uongo? Mungu alikusudia kila mtu aweze kujisomea au kusikiza Biblia mwenyewe na kuielewa.

***Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.***

5. Aliposema Yesu, "Mmesikia ikisemwa..... lakini mimi nawaambia.....," ni mafundisho ya nani aliyokuwa akisahihisha?

a. Mungu Baba
b. Musa
c. Waandishi na Mafarisayo
d. Wanafunzi

6. Kwa nini Mungu alitupatia Sheria?

a. Kutufanya tuwe wenye mashaka
b. Kwa sababu anatupenda
c. Ili serikali zetu zihakikishe mapenzi yake yanatimia
d. Ili tuwakosoe wanaofunja Sheria

7. Yesu alimaanisha nini aliposema wanafunzi wake wanapaswa kuwa wenye haki?

a. Wajiweke sawa kwa Mungu
b. Wawe sawa kwa Mungu
c. Wafanye yaliyo sawa kwa ajili ya Mungu
d. Yote yaliyotajwa hapo juu

8. Tabia yetu ya kiroho inaadhiri vipi uhusiano wetu na watu wengine?

a. Inapaswa kututenga na watu wengine
b. Inaturuhusu kuambia watu vile tulivyo wazuri
c. Tunapaswa kuishi tabia yetu katika uhusiano wetu wote
d. Iko kivyake na haipaswi kuwa na adhari yoyote

9. Yesu anataka sisi tutumie vipi sheria ya Mungu?
    a. Tukumbuke Makusudi na malengo ya Mungu ya sheria
    b. Tukumbuke kuwa sheria ilitengenezwa kwa ajili ya mtu na si mtu kwa ajili ya sheria
    c. Tukumbe kutumia sheria ya Mungu pamoja na upendo wa Mungu
    d. Tukumbuke kugonga watu vichwa kwa sheria ya Mungu

10. Mungu anatwambia tumpende nani?
    a. Familia na marafiki wetu
    b. Wakristo wengine
    c. Maadui zetu
    d. Kila mtu

11. Suluhisho ni nini wakati macho yetu yanatufanya tutende dhambi?
    a. Yang'oe
    b. Jitenge na jumuia kabisa
    c. Tuvae barakoa inayofunika macho yetu
    d. Tuache kutazama chochote kinacho sababisha tutenda dhambi

12. Kwa nini Mungu anapinga uasharati?
    a. Unamadhara mabaya sana kwa wote wanaohusishwa nayo haswa watoto
    b. Unaboromosha famila
    c. Hauelekezi watu kwa uridhisho au utimilifu
    d. Yote yaliyotajwa hapo juu

Unafikiria ni kwa nini mafundisho mengi ya Yesu ni juu ya uhusiano wetu? Je unahusiano wowote: kinandugu, washitaki, wa jinzia tofauti, mwenzi wa ndoa, majirani, au hata maadui, ambao katika huo ni vigumu kudumisha tabia kama za Kristo? Ni katika njia gani mafundisho ya Yesu yanaweza kukusaidia katika uhusiano huo?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwa sababu amechagua kuwa na uhusiano nawe. Muulize akusaidie kukua uwe kama Yesu ili uonyeshe upendo wake kwa watu wengine na uwe sehemu ya suluhisho lake.

**KUZAMA ZAIDI**

1. Ni katika njia zipi Yesu aliwakabili waandishi na Mafarisayo katika fungu hizi sita za Mathayo sura ya 5 zinazoanza kwa maneno yafuatayo "*Mmesikia kwamba imenenwa, lakini mimi nawaambia"?* _____
_____
_____

2. Elezea thamana ambayo Yesu alikuwa akiweka juu ya uhusiano wetu na yule anayemwelezea kama "ndugu" yetu na kwa nini anaweka thamana kuu namna hiyo kwa uhusiano huo. _____
_____
_____
_____

3. Ni vipi na ni kwa nini Yesu anatwambia tukabiliane na majaribu ya ngono? _____
_____
_____
_____

4. Yesu alimaanisha nini aliposema kuhusu kung'oa jicho lako kama kile unachokitazama kinakusababisha kutenda dhambi? _____
_____
_____
_____

5. Kwa nini ni muhimu kwa mwanafunzi wa Yesu kuwa na mfikilio sahihi kwa Sheria (Neno) la Mungu? _____
_____
_____

6. Yesu alifundisha nini kuhusu uhusiano wa mwanafunzi wake na jirani wake na adui? _____
_____
_____
_____

7. Kwa nini Yesu alifundisha kuwa ni muhimu muno kwa mwanafunzi wake kutumia nia za uheri katika uhusiano wake wote? _____
_____
_____
_____